TANGAZO LA SERIKALI NA. 903 la tarehe 01/11/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MAPINDUZI YA MWAKA 2024

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa katika Eneo la Mapinduzi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango Kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Jiji Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO LA UPANGAJI

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ1 yenye majira - nukta 789612MS, 9305220KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS08$^0$MS kwa umbali wa kilomita 2.38 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ2 yenye majira - nukta 789244MS, 9302869KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS73$^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.026 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ3 yenye majira - nukta 788260.55MS, 9302576.61KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS81$^0$MS kwa umbali wa kilomita 0.504 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ4 yenye majira - nukta 787762 MS, 9302648 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ22$^0$'MG kwa umbali wa kilomita

0.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ5 yenye majira - nukta 787537MS, 9303193KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ59$^{0}$'MS kwa umbali wa kilomita 0.881 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPZ6 yenye majira - nukta 788294 MS, 9303642 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazinik - Mashariki katika uelekeo wa KZ39$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 2.056 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
28 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba*
*na Maendeleo ya Makazi*